



**REPUBLIC OF KENYA**  
**COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI**  
**THIRD ASSEMBLY-SECOND SESSION**

**THE HANSARD**

**Tuesday, 31<sup>st</sup> October 2023**

**SPECIAL SITTING**

*(Convened via Kenya Gazette Notice No. 14662 of 24<sup>th</sup> October 2023)*

*The House met at the County Assembly Chamber,  
Malindi Town, at 10:00 a.m.*

*[The Deputy Speaker (Hon. Kombo) in the Chair]*

**PRAYER**

**COMMUNICATION FROM THE CHAIR**

**CONVENING OF SPECIAL SITTING VIA GAZETTE NOTICE NO. 14662 OF 24<sup>TH</sup> OCTOBER 2023**

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): So, hon. Members, we have gathered here for a Special Sitting Pursuant to Standing Order No. 26 (1) to (4) of the County Assembly of Kilifi Standing Orders. It is notified for the information of Members of the County Assembly of Kilifi and the general public that the Assembly shall have a Special Sitting on Tuesday, the 31<sup>st</sup> of October 2023. That is today, as from 10.00 a.m. at the County Assembly Chamber, County Assembly of Kilifi premises situated behind Immigration House in Malindi Town.

The main business to be transacted shall be tabling and consideration of the Report of the Sectoral Committee on Devolution, Public Service and Disaster Management on the Vetting of

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Dr. Francis Fondo who is the nominee to the position of Member, County Public Service Board. Dated 24<sup>th</sup> October 2023. Signed by the Speaker Hon. Teddy Mwambire. Thank you.

### PAPER LAID

REPORT ON THE VETTING OF THE NOMINEE FOR APPOINTMENT TO THE POSITION OF THE COUNTY PUBLIC BOARD MEMBER, DR. FRANCIS FONDO

**Hon. Zia:** Thank you, Mr. Speaker, Sir. Today being Tuesday, 31<sup>st</sup> October 2023, I beg to lay on the Table of this hon. House the Report of the Sectoral Committee on Devolution, Public Service and Disaster Management on the Vetting of the nominee for appointment to the position of County Public Service Board Member, known as Dr. Francis Fondo.

Thank you, Mr. Speaker, Sir.

*(Hon. Zia laid the document on the Table)*

### NOTICE OF MOTION

ADOPTION OF THE REPORT ON THE VETTING OF THE NOMINEE FOR APPOINTMENT TO THE POSITION OF COUNTY PUBLIC SERVICE BOARD MEMBER, DR. FRANCIS FONDO

**Hon. Zia:** Thank you, Mr. Speaker, Sir. I beg to give notice of the following Motion: -

THAT, This House adopts the Report of the Sectoral Committee on Devolution, Public Service and Disaster Management on the vetting of the nominee for appointment to the position of County Public Service Board Member, laid on the Table of this House on Tuesday 31<sup>st</sup> October 2023.

Thank you.

### MOTION

ADOPTION OF THE REPORT ON THE VETTING OF THE NOMINEE FOR APPOINTMENT TO THE POSITION OF COUNTY PUBLIC SERVICE BOARD MEMBER, DR. FRANCIS FONDO

**Hon. Zia:** Thank you, Mr. Speaker, Sir. I beg to Move the following Motion: -

THAT, This House adopts the Report of the Sectoral Committee on Devolution, Public Service and Disaster Management on the vetting of the nominee for appointment to the position of County Public Service Board Member, laid on the Table of this House on Tuesday 31<sup>st</sup> October 2023.

Before I call my seconder, I would like to give my submission. We vetted Dr. Francis Kalama Fondo, and we found that he is suitable for the position. The nominee satisfies the requirements of Chapter Six of the Constitution of Kenya, 2010 on Leadership and Integrity having been cleared by the DCI (Directorate of Criminal Investigation), KRA (Kenya Revenue Authority) on Tax compliance, CRB (Credit Reference Bureau), HELB (Higher Education Loans Board) and EACC (Ethics and Anti-Corruption Commission).

Mr. Speaker, Sir, if Members will adopt this Motion, Dr. Fondo will serve this County as a Board Member. As we speak, the Board is not fully constituted but we have achieved quorum.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Governor will have a duty to bring the other three members who will form the Board. For now, we have Dr. Mturi as the Chairperson, but we do not have a CEO (Chief Executive Officer). We also have Ms. Susan Mumba, Mr. Attas Ali and if we adopt Mr. Fondo then we shall have four members now. I call upon the Governor to bring the other remaining names to the Committee so that we vet them and have a fully constituted Board and start employing our people.

As I was reading the observation that we made as a committee, we found that the nominee has never been charged in a court of law for the last three years. He exceeded the knowledge of topical administrative and technical issues touching on the portfolio to which he had been nominated and has the requisite abilities and qualifications. He has never been dismissed from office under Article 75 of the Constitution of Kenya, 2010 for the contravention of the provision of Article 75(1).

As the Committee, we recommended that having conducted the approval of the nominee and having the suitability, capacity, and integrity of the nominee Pursuant to Section 58(a) of the County Governments Act, 2012, County Assembly Standing Orders No. 43 and the provisions on Public Appointment (County Assemblies) Approval Act No.5 of 2017, the Committee unanimously recommends that this County Assembly of Kilifi approves the nominee.

Mr. Speaker, we found that this person is suitable for the job he was appointed to by the Governor. May I call upon hon. (Ms.) Mariam Mkumbi to second the Motion. Thank you.

**Hon. (Ms.) Mariam:** Thank you, Speaker. I do second.

*(Question proposed)*

**Hon. Rafiki:** Thank you, Hon. Speaker. The Chairperson has already said almost everything. I just wish to support. Thank you.

**Hon. Kubo:** Asante sana, Bw. Spika, kwa nafasi hii. Kwanza, nataka kuipongeza Kamati na kuunga mkono Hoja ambayo iko mbele yetu. Hatujaweza kumaliza kuapisha wote wanaotakikana lakini angalau kazi itanza. Asante.

**Hon. Hinzano:** Asante sana, mheshimiwa Spika, kwa kunipatia nafasi hii. Kabla sijaunga mkono ama kupinga, niko na mapendekezo ambayo kwa kweli ikiwa Kaunti yetu ya Kilifi tulifika katika Bunge hili na kuondoa ile Bodi ambayo ilikuwa inadhalilisha wananchi wa Kilifi, hususan wafanyajikazi ambao walikaa karibu miaka sita hadi nane wakiwa hawajaajiriwa, ni vibarua. Tukaamua kuvunja hiyo Bodi ili tuhakikishe kwamba tunaweka sawa mambo ambayo yanaendelea katika ufanyajikazi hapa Kilifi. Tulifanya hivyo, lakini baada ya muda tukasikia kuna watu wanaajiriwa na hiyo Bodi ilikuwa imevunjwa. Kuna vijana wanaajiriwa ambao wanachukua nafasi za kazi ambalo ni jambo zuri lakini hatujui kama Bunge tulipovunja ni kwamba kila kitu kilisimama kwa sababu kulikuwa hakuna ile Bodi ambayo ingeweza kuangalia wafanyajikazi wa Kaunti yetu.

Hivi sasa, hili jina tukilipitisha kuna sababu ya kwamba kutakuwa kuna mtu wa kuulizwa kwa sababu tutakuwa tunajua huyu Mwenyekiti ambaye atakuwa hapo na hiyo Kamati yake...

*(Hon. Koki stood on a Point of Order)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Mheshimiwa Morris (Hinzano) tungetaka kumsikia mheshimiwa Koki kama ana mawazo gani.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

**Hon. (Ms.) Koki:** Asante, mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii. Hii ni Nyumba ya heshima na inaheshimika na tuko katika mitandao na wananchi wa Kilifi wanatuona. Ni vizuri kwa kiongozi aliye Sakafuni atuambie ni vijana gani walioandikwa na kama anao ushahidi wa vijana walioandikwa kwa sababu mimi nakaa katika Kamati hiyo na hatujawahi kuambiwa kama kuna ajira zozote ambazo zimetoka. Ni vizuri anapozungumza, azungumze akiwa na ushahidi ndio kama Kamati tufuatilie. Asante.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Mheshimiwa Morris (Hinzano), kulingana na alivyouliza mheshimiwa Koki, je uko na uthibitisho ya kwamba kuna vijana waliandikwa kazi?

**Hon. Hinzano:** Asante sana, mheshimiwa Spika. Nina akili yangu timamu na siwezi kusimama katika Bunge hili kuongea jambo ambalo halipo na sitaweza kufanya hivyo...

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Swali ni unacho kithibitisho ambacho unaweza kukileta hapa mbele na kama hauna uweze kuondoa hiyo kauli.

**Hon. Hinzano:** Ninacho kithibitisho lakini kwa muda nitaleta kwa sababu hata katika wadi yangu kuna vijana ambao waliandikwa kazi ambapo wanafanya kazi, kwa hivyo ushahidi ninao.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Sasa kwa sababu ya wakati huu hauna ushahidi, tafadhali toa hiyo kauli.

**Hon. Hinzano:** Asante sana. Kwa heshima yako ninaondoa lakini nitaleta ushahidi kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Nikisimama hapa ningepomba Bunge hili tukufu kuweza kufanya haraka hata pia hao wengine watatu ambao pia hawajaweza kuteuliwa, Gavana aweze kufanya haraka ili kuhakikisha kwamba hii tume imekamiliwa ili kwamba tuwe na mtu wa kuuliza kwa sababu Mwenyekiti huyu ambaye tunaenda kumpitisha na naomba Bunge limpitishe kwa haraka sana kwa sababu kama wabunge wa Kaunti lazima tuwe tuna mtu wa kuuliza.

Kwa hivyo, nataka nipongeze Kamati kwa juhudi zenu za kupitisha hili jina kwa sababu huu ndio mwanzo wa kuweka mambo sawa katika Kaunti yetu ya Kilifi. Naunga mkono asilimia mia moja hili jina tulipitishie ili kuweza kuhakikisha ya kwamba Kaunti yetu ya Kilifi kila kitu kinawekwa sawa na kumsaidia Gavana kwa sababu Gavana peke yake hawezi kufanya. Lakini, Tume hii ikishikana vizuri na wahusika wa Kamati yetu hapa Bungeni na wale washikilizi wa maofisi katika Kaunti yetu ya Kilifi, basi hata Gavana itatoka ile picha kwamba zile ahadi zake ambazo ameziweka zinaweza kutekelezwa na ni ajira kwa vijana kama mpangilio wake yuko nao kwa Kaunti yetu.

Kwa hivyo, tuhakikishe kwamba jina linapita ili tumpatie nguvu Gavana na majina ambayo mheshimiwa Koki anayahitaji. Asante.

**Hon. Shehe:** Asante, mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii. Nataka niwapongeze wale ambao wamepitisha jina hili la huyu bwana ambaye yuko kwa Ripoti tuliyo nayo. Masomo ni sawasawa na kadri ya maelezo ya mheshimiwa *Chairman* alivyosema inaonekana tunao watu ambao wanaweza kuhudumu katika eneo letu la Kaunti ya Kilifi.

Bw. Spika, nataka tujihadhari kabisa tupeanapo madaraka kama haya. Wawe waangalifu hawa tunawapatia madaraka kwa sababu madaraka kama haya wale waliokuweco walipitia viwango vya *vetting* kama hivi na baadaye wakabadilika wakawa ni watu ambao wanaenda kinyume na hali ya mapendekezo yaliyokuwa yanatakikana katika himaya yetu ya Kilifi.

Ni pongezi tukiona mtu amefika kiwango kama hiki na amepewa hiyo nafasi lakini hizi nafasi wazitumie kwa uangalifu maanake watu wameteseka kwa muda mrefu. Wengine waliokuwa wakitarajia kuandikwa imekuwa ni kama mambo ya maneno tu. Unapewa nafasi ya kuenda kufanya kazi na hupewi mshahara miezi na miaka. Wengine wameketi karibu miaka tisa hawajapata hata karatasi ya uthibitisho kwamba anafanya kazi wapi. Kwa hivyo, sisi tukiwa tuko

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

hapa kama *overseers*, ningomba tuwapatie hiyo nafasi kwa uharaka. Pongezi kwa watu wetu wa Kamati husika na tutarajie kwamba mambo yataenda sambamba. Langu ni hilo, Bw. Spika. Asante.

**Hon. (Ms.) Koki:** Thank you, Mr. Speaker. As one of the Members of the Committee who vetted Dr. Fondo, we found out that Dr. Fondo has a lot of wisdom. His education and the exposure that he has from public and private institutions proved to the Committee that he is the right candidate for the job. The Committee was happy during the vetting with how he was responding to the questions. All I ask for in this House is to pass this name so that the Board can be able to start working as we wait for three Members to come for vetting because a lot is at a standstill because until now no employment is going on.

Those that are working as casuals have not been confirmed. There is so much that needs to be done and it cannot be done until this Board is fully constituted. So, I urge the hon. Members to pass this name so that this Committee even though we are still waiting for the three members, can already start working so that even the youth, women and people living with disability in Mariakani can also get opportunities to work for this county and be part of the county. Thank you, Mr. Speaker.

**Hon. (Ms.) Betty:** Asante sana, mheshimiwa Spika. Ninayo furaha kuu kwa sababu siku ya leo ni siku yangu ya kuzaliwa. Pia, naunga mkono kupitisha bwana ambaye atakuwa akisimamia maswala ya Bodi. Kama unavyojua, mimi hapa ndani ninawakilisha vijana wa Kilifi Kaunti na huko nje vilio vya ajira vimekuwa donda sugu. Ninacho amini na ninacho tamani ni kwamba huyu ambaye ataenda kupatiwa hii nafasi ataweza kutekeleza majukumu yake kwa usawa na uhaki. Isiwe kama ni mbinu mtu yeyote atakayepatiwa mamlaka aweze kuchezea, aandike watu anao wajua au kwa kutumia rushwa. Haya ni mambo ambayo sisi kama Bunge tuyakemee na ikiwa kuna kitu chochote ambacho kitatokea ambacho wananchi wa Kilifi hawatafurahia basi pia huyu naye acha niseme wembe ni ule ule.

Tuko hapa kuwakilisha watu wetu wa Kilifi ili tuweze kusonga mbele. Kwa hivyo, mheshimiwa Spika, vitu vingi ambavyo vilikuwa vimesimama saa hii ninayo imani kuwa vitaendelea. Vijana wetu wa Kilifi Kaunti waweze kupata ajira na waweze kujimudu. Mambo ya mihadarati na wizi mitaani iweze kupungua. Asante sana.

**The Deputy Speaker (Hon. Kombo):** Asante sana na pongezi kwa siku yako ya kuzaliwa mheshimiwa.

**Hon. (Ms.) Grace:** Asante, Bw. Spika kwa kunipatia fursa hii. Kwanza, ningetaka kumtakia Mheshimiwa Betty Kache siku njema ya kuzaliwa.

Pili, nataka kupongeza Kamati ya *Devolution* kwa kazi nzuri waliyoifanya na ninaunga mkono uteuzi wa Francis Kalama Fondo. Wazungu wanasema this *appointment was long overdue*. Kuna kilio huko nje watu wa Kilifi wanataka kazi na hizi kazi hawawezi pata bila *process ya Public Service Board*. Kwa hivyo, ninaunga mkono uteuzi wa Kalama na ninarudia maneno ambayo yametamkwa na mheshimiwa Betty kwamba tunawaangalia na wakienda kinyume na matarajio ya wana Kilifi mambo ni matatu na wembe ni ule ule.

**Hon. Mohamed:** Asante, Bw. Spika, kwa kuweza kunipatia fursa hii ili pia niweze kupeana maoni yangu. Nataka kuungana na wezangu kumtakia mheshimiwa Betty heri ya kuzaliwa na Mungu amjalie.

Pili, nataka kuungana na Bunge hili kuweza kuunga mkono uteuzi wa Bw. Fondo kama mmoja kati ya wanachama wa Bodi ya Uajiri Kilifi. Bodi hii tulikuja tukavunja hapa ni muda kwa sasa na Kilifi imekaa bila bodi na ajira imekuwa haiwezi kupatikana.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Kwa hivyo, mimi pia ningependa kuungana na mshimiwa Morris (Hinzano) kwamba ni muhimu upande wa serikali kwamba tuweze kumshauri mstahiki Gavana iwezekanavyo. Wale wengine watatu walio baki waweze kuletwa ili tupitishwe bodi hii iweze kusimama kidete na kuanza kuajiri wakaazi wa Kilifi, maanake ni mwaka karibu wa kwanza unaenda kuisha sasa kutoka serikali hii iingie mamlakani na imekuwa kwamba wale tuliwapata wakiwa kama wafanyikazi ambao sio wafanyikazi walioajiriwa, Kizungu unaweza sema *permanent* wako *contract* basi mpaka leo bado wako *contract*. Kwa hivyo, tuko na jukumu kama Bunge, serikali ina jukumu pia kuhakikisha kwamba bodi hii inasimama haraka iwezekanavyo. Nasimama kuunga mkono uteuzi wa Bw. Fondo.

**Hon. Juma:** Asante, Bw. Spika, kwa kunipatia nafasi hii na mimi kuchangia mambo ya Bw. Francis Fondo. Bwana huyu mimi simjui moja kwa moja lakini nimepekua makaratasi yake hapa na nimeona kwamba Wajumbe wote wa ile Kamati husika wana tajriba ya kutosha ya kuweza kumpatia hiyo nafasi kama wanavyozungumzia hapa.

Jambo ambalo naomba kusisitiza ni kwamba si makaratsi ya mambo ya masomo pekee tuweze kumweka afisa fulani mahali fulani bali pia tuangalie mambo mengine, maanake wale waliotangulia wengine walikuwa labda wana tajriba na wana makaratsi ya kutosha kumshinda hata bwana Francis. Lakini baadaye tukaona kama ambaye jamii yetu katika njia moja ama nyingine wanaponzwa, kwa hivyo sasa hivi sisi kama Wajumbe ni tusilale. Ikizidi miaka mitatu kama kuna mahali tunaona hakuendi sawa tuweze kukaa kama Wajumbe...

*(Hon. Grace stood on a Point of Order)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Mshimiwa, wacha tumpe nafasi mshimiwa Grace, tuone yuko na lipi la kusema?

**Hon. (Ms.) Grace:** Asante, Bw. Spika. Ningependa kumuuliza mshimiwa ambaye yuko Sakafuni atuelezee mambo hayo mengine ambayo anasema yaangaliwe. Atufafanulie ni mambo gani?

**Hon. Juma:** Asante, labda mienendo ya kule anakoishi, tabia zake na mambo kama yale. Maanake hapa tumeonyeshwa makaratsi labda ya shule peke yake. Kwa hivyo, mienendo kule kwa jamii alikuwa akiishi vipi, ndio tuweze kumpatia mikoba kisawa sawa.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Nafikiri mshimiwa Juma, hapo utakuwa unatoka nje ya maswala kwa sababu Kamati ile iliyomkalisha ilianguzia haya yote na waliweza kumuuliza maswali yote ambayo yalikuwa yanaambatana na yeye na vile anvyoishi. Mimi nafikiri uwe na imani kwamba Kamati ilifanya kazi nzuri.

**Hon. Juma:** Ndio nimesisitiza na nikapongeza kwamba Kamati ya Bunge hili ina tajriba na imeweza kufanya vilivyo sawa kabisa. Nikasema siku zijazo tutakuwa ngangari; sisi ni vioo vya jamii. Tuhakikishe hatuanguzii makaratsi tu lakini nyumbani tumwanguzie ili atakapopata nafasi hiyo afanyie kazi jamii. Nikaongezea kwamba ndani ya miaka mitatu kama tunaona mambo hayaendi vizuri, basi tuwe macho ili tuweze kuwaweka kando na kutafuta watu ambao watusaidia. Kwa hivyo, hili pia nilikuwa naona niliwasilishe. Asante, Bwana Spika.

**Hon. Kea:** Asante sana, Spika wetu. Mshimiwa Betty Kache, *congratulations and happy birthday*. Leo mimi nasimama hapa kuafikiana na wenzangu kwa huu uteuzi wa Bw. Fondo. Kitu kimoja tu ambacho kinanisikitisha ni kwamba sijui kwa nini hatukuletewa majina yote na tukapitisha kwa pamoja ili hili jambo tuwe tumelimaliza mara moja.

Bwana Fondo namjua mimi mwenyewe binafsi katika kituo chake cha afya pale Kilifi na kazi yote ambayo amekuwa akifanya hasa kusaidia watu wa Kilifi. Mwenzangu alikuwa

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

amesema kwamba akiiba lugha ile ya mayai ya kwamba “*it was long overdue*” ni kweli kwa sababu kuna kundi la kwanza lilikuja likapitishwa katika Bunge hili na huyu akabaki na imechukua muda mpaka leo sasa tuko hapa kufanya hayo mambo ya kupitisha na kisha tutarudi tena kwa mara ya tatu kupitisha wale wengine watatu.

Ombi langu tu ni kwamba ile Kamati ambayo inahusika na mambo kama haya ikiongozwa na Mwenyekiti wetu ambaye ni mchapa kazi vizuri, haya majina mengine yafike kwa mapema ili tuje tumalize. Lakini uteuzi wa Bw. Fondo ninauafiki asilimia mia moja kwa sababu anafaa kabisa katika hii nafasi ambayo amepatiwa.

Lengine ni kwamba kuangalia na hali ya Bunge hii ni kwamba wengi tunaafikiana kwa hili jambo la kumpitisha Bw. Fondo. Kwa hivyo, nikawa ninauliza kama itawezekana arudi kwa Sakafu Mwenyekiti wa Kamati ili atetee kidogo kisha halafu swali liulizwe na tupitische kwa umoja. Asante sana.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Mheshimiwa Moses Furaha (Kea), wenzako wote wamepewa nafasi wakajadili vizuri na kutoa maoni yao bila kufungia wenzao lakini wewe unaonekana umechukua nafasi hii kutaka kufungia wengine.

*(Laughter)*

Kwa sababu ya umri na heshima, wacha tuende na neno lako kwamba tumpe Mwenyekiti wa Kamati ya Ugatuzi aweze kutufungia huu Mjadala.

**Hon. Zia:** Asante sana, mheshimiwa Spika.

*(Hon. Zia spoke off record)*

Hivi vitu vinatakikana vitengenezwe vizuri kwa sababu, sasa vinaanza kuleta shida katika hili Bunge. Mwenyekiti wa ICT fanya kazi. Bunge hili liko na heshima zake na napongeza sana kwa yale yote ambayo yamewezwa kujadiliwa hapa.

Mheshimiwa Moses Furaha (Kea) amesema nitetee, nitetee nini?

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Mheshimiwa, umepewa nafasi ya kumaliza huu mjadala.

**Hon. Zia:** Ni sawa, wacha nishukuru Wabunge wenzangu ambao wameweza kujadili na wale ambao hawakuweza kujadili kwa kuweza kufika na kujadili hili swala la hii Ripoti ambayo tumeweza kuitayarisha. Pongezi sana na Mungu awabariki.

Dada wa Bunge hili, kitinda mimba wetu *happy birthday* na nimekutunuku kwa keki kwa hivyo wabunge wote tutakula.

*(Hon. Rafiki stood on a Point of Order)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Mheshimiwa Justin Rafiki.

**Hon. Rafiki:** Asante, mheshimiwa Spika. Ningeomba labda mheshimiwa Mwenyekiti ambaye anaongea atueleze vizuri maanake nimemsikia akitoa shukrani kwa wadada wa Bunge hili...

*(Laughter)*

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Nimemskiza vizuri. Tafadhali mheshimiwa Spika, muulize atueleze maana akisema wadada wa Bunge hili...

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Mheshimiwa Justin Rafiki naona tumpe nafasi Mwenyekiti aweze kumalizia mazungumzo.

**Hon. Zia:** Sawa, wacha nifunge. Asante sana, kwa kunitetea, mheshimiwa Spika. Nashukuru Bunge kwa yale yote ambayo mmeweza kuyajadili. Nyinyi ni wa maana na Mungu awabariki. Nawatakia *recess* nzuri na Mungu awazidishie mpate baraka na neema zake. Asante sana.

*(Question put and agreed to)*

### ADJOURNMENT

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Hon. Members, there being no other agenda for today, this House stands adjourned until further notice. Thank you.

The House rose at 10:39 a.m.